

**Dondoo za mkutano wa Umma wa Wapanda Baisikeli Dar es Salaam
1 Agosti 2009**

Waliohudhuria

Juma Ali Salehe Jongo
Shamte J Kisoma
Mohammed Samwely
Sosthenes C Amlima
Selion Elieskia
Abdul H Mwaibambe
Filbert Mbecha
Athumani Mussa Kitemo
Paulo Atibu Hatibu
Mohammed Kasimu Kipende
Hamadi Hatibu Bwaja

Turning Point DVD

Sosthenes Amlima ametoa wazo kuhusu video ya DVD ya usalama barabarani ya Turning Point ambayo tulipata Kempinski tuweze kubadilisha kutoka kiingereza kwenda Kiswahili, ili tuweze kuiga na kuandaa video yetu ya usalama barabarani kwani video hiyo ni nzuri inafaa kama tutaiga.

Mafunzo ya kiingereza

Mafunzo ya lugha ya kiingereza, Jumapili ya tarehe 26/07/09 hatujaweza kujifunza kwa sababu Juma S Jongo alifunga ofisi na kuondoka na ufunguo bila taarifa. Na jumamosi ya tarehe 1/08/09 hatujaweza kujifunza kwa sababu mwalimu ana sumbuliwa na homa.

Marekebisho ya barabara

Fomu ya kujaza matatizo mbali mbali ya barabarani tunasubiri zitolewe copy nyingi ili kila mwanachama aweza kupata.

Kufuri za ofisi

Tumekubaliana mkutano wa tarehe 15/08/09 tutanunua kufuri mpya za ofisi mbili ambazo zitakuwa na funguo tatu kila kufli ili tuweze kugawana kati ya Juma, Filbert na Elaine ili kondokana na usumbufu wa kumtegemea mtu mmoja kutunza funguo.

Uchaguzi wa 2010

Usambazaji wa barua za kuomba ilani ya uchaguzi Paulo Hatibu amepeleka Chama cha TLP, CHADEMA, NCCR, CCM, CUF bado vyama vingine inabidi kuviandikia barua za kuomba ilani zao.

Msafara

Juma amesambaza barua za British High Commission, Embassy of Ireland, Embassy of Japan na wameweza kutoa namba zao za mawasiliano isipokuwa Embassy of Ireland wamesema tu wasiliane nao kuanzia mwezi wa nane muhusika atakuwa amerudi likizo. Bado Netherlands, Swede, Danish na ubalozi wa China Mejah anayo alipewa na Juma ili apelike.

Shirika la Fasta cycle couriers

Tutakuwa na mkutano na Bwana Bukuku na pia ni siku ya uchaguzi baada ya kuongea na Bukuku tarehe 15/08/09.

Re-cycle

TRA Mejah anafuatalia.

Hela na guta

Hela ya guta, Filbert alibakiwa na Tsh 15,000 ya guta. Dereva wa guta anadaiwa jumla ya Tsh 18,000 ya wiki iliyopita Tsh 11,000 na wiki ya leo hii Tsh 7,000.

Posho ya Juma S Jongo tarehe 26/07/09 Juma alipewa malipo ya Tsh 5,000 kama malipo ya awali (advance) na tarehe 1/08/09 amelipwa Tsh 15,000 kwa hiyo jumla Juma amelipwa posho yake yote Tsh 20,000 ya mwezi wa saba. Kwa hiyo Filbert hana pesa ya guta Tsh 15,000 aliyokuwa nayo amemlipa Juma.